# MPATE TU KRISTO NDANI YA MOYO, MENGINE YOTE YATASHUGHULIKIWA

*………Manadhihirishwa kwamba mmekuwa barua ya Kristo tuliyoikatibu, iliyoandikwa si kwa wino, bali kwa Roho wa Mungu aliye hai si katika vibao vya mawe, ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama (2kor 3:1-6)*

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema juu ya hilo. Nimepita tu tarehe yangu ya kuzaliwa siku ya jumaatatu, na nilikuwa na miaka hamsini na mitano. Na unajua ile familia ya Branham kamwe hawa kuniomba nijiunge na familia yao. Nilizaliwa nikiwa ni Branham, na hivyo ndivyo tulivyo wakristo tumezaliwa tu tukiwa wakristo kwa nguvu ya ufufuo ya Yesu Kristo na sisi ni wakristo kwa kuzaliwa (Yohana 3: 1-8) hiyo inatufanya sisi kuwa ni viumbe vipya (wagalatia 6:15 16) katika asili yetu ya zamani hatungeweza kuwa wakristo. Hivyo ndiyo sababu leo tunao wengi wanaojiita ni Wakristo, na wakiishi maisha ya aina yoyote ile. kwamba hawakupata ule uzoefu wa kuzaliwa mara ya pili, kitu kile ambacho kinakubadilisha wewe, ambacho kina uondoa uhai nje kama vile kutoa damu kutoka ndani ya mtu aliye na aina fulani ya damu, na kuweka aina nyingine ya damu ndani yake. Ni kutoa ule uhai wa zamani kutoka ndani ya mtu na kuingiza uhai wa Kristo ndani ya mwamini. Hapo sasa anakuwa kiumbe kipya (2kor 5:17) anakuwa kiumbe kipya [1]

Kumbuka Biblia ilisema “Ninyi ni barua zilizo hai zinazosomwa na watu wote” (2koro 3:2) sasa watu wengi hawatasoma Biblia lakini Mungu amewafanya ninyi kuwa wawakilishi wake hai. Ni barua inayotembea unapaswa uwe ni Bblia inayotembea, kristo ndani yako unapaswa kuwa neno la Mungu linalotembea. Na kama unasema umkristo na siyo hivyo, ushawishi wako, kile unacho shawishi kitu kulazimu uje kujibu kwa nafsi nyingi ulizoziacha pembeni zisiwe za kmfuata Kristo katika siku ile ya hukumu.

Tunajua ya kuwa mtu lazima afe na baada ya hapo hukumu (waebrania 9:27 - 28), kifo siyo kitu kigumu, ni hukumu baada ya kifo ndiyo sehemu mbaya. Na pale yale uliyoyafanya katika maisha na vile ulivyo washawishi wengine itabidi ujibu kwa hayo katika siku ile (2kor 5: 10 - 11)

Ni kwa kiasi gani tunapaswa kuweka pembeni kila mzigo na dhambi ituzingayo kwa upesi na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tusiangalie kanuni na madhehebu au kwa mtu mwingine ila Yesu Kristo ambaye ni mwanzilishi na mkamilishaji wa Imani yetu (Waebrania 12: 1- 3) [2]

Usidanganyike ni vizuri ukilichunguza kwa karibu sasa unaona, ama utaendelea kusema “Vema usinilaani mimi kufanya hivi, na hainihukumu mimi kufanya hivi” mambo ya dunia? Sasa nitaenda kuwaumiza ninyi kidogo, kuyasukumia manyoya upande wa pili lakini huo ni ushahidi wa uhakika kwamba, kamwe hujakutana na Kristo kamwe hujazaliwa mara ya pili. Yeye apendaye dunia na mambo ya dunia upendo wa Mungu haumo ndani yake (1Yohana 2:15-17)

Sasa kama utaacha kufanya hicho kwa sababu unajua unapaswa kuacha hicho, kwa sababu unajua unapaswa kuacha hicho, na unaacha kufanya hiki, hivyo ni ishara kuwa kujafika mahali popote bado. Wakati hicho kitu kinapo kuwa kimekufa ndani yako, na ile ya asili ya hicho imetoka ndani kuna mtu mwingine ndani pale na inaweza tu kuwa……… Roho Mtakatifu Yule aliyekuwa ndani ya Kristo alikuwa ndani yako atazaa/ataleta uhai utakaofanana kama wa Kristo. Hakuna unachofanya ni kile alichofanya alichagua hicho kabla ya kuwekwa misingi ya dunia. [3]

Usijaribu kuwa na misisimko yoyote, chochote cha kuchukuwa mahali pa Roho Mtakatifu kule kuzaliwa mara ya pili kunapokuja umebadilishwa kuthibitisha hili, kwa maisha yako, upendo wako amani, uvumilivu, upole, utu wema, subira, hivyo ndivyo ulivyo (wagalatia 5:22) na dunia yote inaona kielelezo/kuakisi kwa Yesu Kristo ndani yako [4]

Hebu na tusiangalie mambo makubwa na tumuone Kristo katika maisha yetu. Hebu tuangalie unyenyekevu unaona? (warumi 12:16) [5]

Na inatubidi siku zote tujaribu kumweleza/kumuakisi Kristo katika maisha yetu na kila kitu tufanyacho [6]

Yeye aliye ndani yenu ni mkuu, kuliko aliye katika dunia (1Yohana 4:4) ni kitu gani kiko ndani yenu? Ni Kristo mpakwa mafuta, Mungu aliyekuwa ndani ya Kristo yuko ndani yenu, [8]

Roho Mtakatifu ni Yesu Kristo katika umbo lingine, hiyo ni kweli [7]

Sasa kama yuko ndani yako (wagalatia 2:19-21) unaona? Siyo kuwaza kwako na vile uwezavyo kuwaza juu ya hilo ndani yako, yeye kwa hakika hawezi kukanusha kile alichosema na anajaribu kumfuata mtu Yule ambaye yeye anaweza kujithibitisha mwenyewe kupitia huyo.

Hivyo sasa vipi kuhusu uponyaji wa wagonjwa? Unaona? Yeye aliye ndani yenu ni mkuu kuliko ugonjwa unaona? Kwasababu hiyo kuingilia unaingilia hasa sheria za Mungu ndio ugonjwa ulivyo. Au Yeye aliye ndani ni mkuu, Yeye mponyaji na Muumbaji, kuliko shetani ambaye ameingilia utaratibu wa maisha yako (1petro 2:21-24)

Lakini yeye aliye ndani yako ni Kristo. Na kama Kristo yuko ndani yako, kazi za Kristo utazifanya kama Kristo anaishi ndani yako, alisema hivyo (Mt Yohana 14:12) “Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo atazifanya pia” kama ungekuwa ndani ya Kristo au kama Kristo anaishi ndani yako…. Hapo sasa Kristo ni Neno. Ni sawa? Na Neno linakuja kwa manabii wake (Amosi 3:7) unaona? Na kama Kristo anaishi ndani yako kazi za Kristo zitaishi kupitia wewe. Kazi alizofanya, maisha aliyoishi na kila kitu vitaishi ndani yako.

Lakini kama bado unaishi maisha yako mwenyewe hapo sasa kazi zako mwenyewe utazifanya (waebrania 4:10-11) kama una shaka na kushuka juu ya ahadi za Mungu zilivyo, hapo sasa Kristo hayupo hapo. Kama Kristo anaishi ndani yako, Neno lake atalitambua na ahadi zake atazitenda. Unaona? Atazifanya [8]

Tunapokuwa ndani ya Kristo tunakuwa na Baraka za kiroho (waefeso 1:3). Tukiwa nje ya Kristo tunakuwa na misisimko. Katika Kristo tunabaraka halisi sio za kujifanya, za kuingiza za kujipachika. Lakini ili mradi unajaribu kusema kuwa uko katika nchi ya ahadi, na hauko, dhambi zako zitakutafuta, lakini unapokuwa ndani ya Kristo Yesu, amekuahidi wewe amani ya mbinguni (Yohana 14:25) Baraka za mbinguni, roho wa kimbinguni vyote ni vyako (1 Kor 3:21 - 23). Uko katika nchi ya ahadi na katika umiliki mkamilifu wa kila kitu Amen. Jinsi ilivyo nzuri. [9]

Na kama Neno likikaa ndani yako hapo sasa wewe ni mtu aliyepakwa mafuta na Neno “mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni lolote mtakalo nanyi mtatendewa” (Yohana 15:7). Huyo ni Kristo ndani yako akilipaka mafuta Neno la wakati huu, kwa wakati wowote walioishi [10]

Njia pekee ambayo unaweza kuishi maisha yanayoistahili injili ndani yako na kuzionyesha/kuakisi zile ahadi zake pale nyuma ili zifanye/ zithibitishwe. Muache Mungu aishi ndani yako azithibitishe ahadi za siku yako ya leo kama vile tuu Yesu alivyomwambia Yohana” kubali hivi sasa Yohana hiyo ni kweli lakini sisi ni wajumbe wa siku ya leo kwa kuwa ndiyo itupasavyo kutimiza haki yote (matayo 3:13-15). Na kama sisi ni wakristo wa siku ya leo hebu tumpokee Yesu Kristo ndani ya mioyo yetu.(Yohana 1:12-15) na Yesu ni Neno usipinge/kukataa hata moja sema ni kweli. Na uliweke hilo moyoni mwako na uangalie lile tunda la Roho juu yako, na kutimiza kila ahadi ambayo ameiweka katika Biblia. Mungu anapenda kutimiza Neno lake na y eye hana mikono yoyote ila yangu na yako. Hana macho yoyote ila yangu na yako, hana ulimi wowote ila wangu na wako “Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi” (Yohana 15: 1- 15) yale matawi ndiyo yazaayo matunda, ule mzabibu hutia nguvu matawi hayo ni maisha yastahiliyo. [11]

Kila dhehebu litazaa maisha yake yenyewe. Lakini kama ile mbegu ya asili itaenda kutoa tawi lingine litazaa zabibu kama lilivyofanya wakati wa mwanzo, na kama uhai wa Yesu Kristo utaenda kuleta mwili mwingine wa waaminio utazaa matunda yote yale kama ule wa kwanza ulivyofanya wataandika kitabu cha matendo ya mitume nyuma ya kile kwa sababu itakuwa ni uhai uleule, unaona ninacho maanisha huwezi ukaenda mbali na hilo ni uhai wa Kristo ndani yako ukiwa umeingizwa ndani yako na Roho Mtakatifu mwenyewe [12]

Na kumbuka aliwakataza wanafunzi wasiendelee tena kuhubiri kutenda chochote mpaka wapate nguvu za Roho kaeni mjini hata mvikwe uwezo utokao juu” (Luka 24:42-49) unaona? Hapa si kwenda nje mpaka iwe siyo wewe ila Mungu, watu waweze kuona kule kumwakisi Yesu Kristo ndani yako hapo sasa watu wataamini kwasababu siyo wewe, itakuwa ni Yeye na wale wote aliowajua kimbele atawaita (Rumi 8:30) wataliona hilo “ Kondoo wangu wanaijua sauti yangu” [13]

Hatuhitaji kuwa na kusanyiko kubwa hatulazimiki kuhubiri kwa makumi elfu. Hatulazimiki hata kule kuhubiri tunaweza tukawa ubao wa matangazo wa Mungu (2 kor 3:1-3) unajuaje kuwa maisha yako yanaweza kumfanya kijana mdogo aanze kufuata injili baadhi ya ninyi wanaume wazima/wazee ninyi wanawake wazima/wazee kufanya vijana wadogo wanaume waende shamba kwa Bwana kuwaleta makumi elfu kwa Kristo ni kwa sababu alimuona Kristo ndani yako. Ni wewe uliyemwonyesha Kristo kwake kwa maisha rahisi ya nguvu za injili

Ndiyo nafikiri tunamhitaji Kristo ndiyo Bwana, njia pekee tuwezayo kumuona Kristo ni pale anapojiakisi kwa kila mmoja wetu. Namuona Kristo ndani yako unamwona Kristo ndani yangu, hivyo ndivyo tumuangaliavyo Kristo [14]

Wa zamani huu mti wa zamani wa kale uliopo katika maana haya hushikilia majani yake wakati wote wa baridi wakati wa wewe achia tuu ule uhai nje ndani lile jani la zamani linadondoka. Hivyo ndivyo ilivyo muachie Kristo aje ndani ya mioyo yale yaliyoandaliwa yatajishughulikia yenyewe hivyo ni kweli mwache tu Kristo aje moyoni mambo mengine yatajishughulikia yenyewe.

NUKUU ZA KIINGEREZA

[1] Kristo alivyojitambulisha katika nyakati zote (64 0409) aya E-23
[2] Ushawishi (64 - 0215) Aya 26 29
[3] Israel kule misri (53 0325) Aya 63 – 65
[4] Waebrania sura 5 na 6 (53 - 0908) Aya 189/136 – 138
[5] Utambulisho (63 – 123) aya E-100
[6] Ushawishi 63 – 0112, Aya E-14
[7] Ule muhuri wa kwanza (63 – 0318) kitabu cha mihuri uk 157

[8] Yeye aliye ndani yenu (63 – 1110E) Aya 153+154+182+187+188

[9] Wana wa Mungu waliodhihirishwa (60 - 0518), aya 36
[10] Tumeona nyota yake (63 1216) Aya 147
[11] Je maisha yako yanaishahili injili (63 0630E) Aya 272
[12] Kristo ni siri ya Mungu iliyofunuliwa (63-0728), uk 44
[13] Yesu Kristo Yule Yule (63 - 0604) Aya E-42
[14] Acheni nuru yenu iangaze mbele za watu (61 - 0903) Aya E – 51
[15] Unamini hili? (50 - 0716), Aya 59

*Jiwe la kiroho la kujengea na 02 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii. Iliyokusanywa na Gerd Rodewald Friedenstr. 69-D– 75328 Schomberg Germany Simu (+49) 7235 - 7613. Fax (+49) 7235 3306.*

*Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itaizunguka dunia, zile mbegu zitaingizwa magazetini na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo na mafundisho uk 724)*

*Kwa nakala zaidi za kiingereza na kiswahili. Andika kwa: Charles E. Y. Kanju*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*